

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**  
**JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**



**KUITWA KWENYE USAILI**

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji anapenda kuwatangazia kuwa vijana waliomba ajira ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuitia mfumo wa ajira ZIMAMOTO RECRUITMENT ([ajira.zimamoto.go.tz](http://ajira.zimamoto.go.tz)), Usaili utafanyika kuanzia tarehe **05 Aprili, 2025** hadi **tarehe 17 Aprili, 2025** kuanzia **saa 1:00 Asubuhi** kwa kila kundi.

Waombaji waliomba ajira kwa elimu ya kidato cha nne usaili wao utafanyika kuanzia tarehe **05 hadi 09 Aprili, 2025 saa 1:00 Asubuhi** kwenye mikoa walioichagua wakati wa kutuma maombi.

Waombaji wenye elimu ya Shahada na taaluma mbalimbali usaili wao utafanyika katika Ukumbi wa Andengeny - Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Dodoma kuanzia tarehe **14 Aprili hadi 17 Aprili, 2025 saa 1:00 Asubuhi** kwa kila kundi.

Zingatia yafuatayo:

- i. Kila mmoja anatakiwa kufika kwenye usaili siku na tarehe aliyopangiwa na si vinginevyo.
- ii. Kuwa nadhifu na kucaa mavazi ya staha.
- iii. Kufika na vyeti vyote halisi vilivytumika kwenye maombi ya ajira kama vile cheti cha Kidato cha nne, Kidato cha sita, Cheti cha taaluma, cheti cha kuzaliwa, pamoja na Kitambulisho cha Taifa au Namba ya kitambulisho cha Taifa (**NIDA**)
- iv. Kwa walioomba nafasi ya Udereva pamoja na maelekezo hayo wanatakiwa kuja na leseni halisi ya udereva **Daraja E.**

- v. Gharama za usafiri, chakula na malazi ni juu ya msailiwa kwa muda wote atakaokuwa kwenye usaili.

Vijana watakaofanya usaili Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wazingatie tarehe zao za usaili. Aidha, atakayekuja tarehe ambayo haijapangwa hatapokelewa.

Orodha ya Vijana waliochaguliwa kufanya usaili pamoja na makundi hayo inapatikana katika tangazo hili kuitia tovuti ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ([www.zimamoto.go.tz](http://www.zimamoto.go.tz))

*Imetolewa na;*

Kamishna Jenerali

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Makao Makuu Dodoma

**30 Machi, 2025**